**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania...**

Ni furaha kujumuika pamoja katika hafla ya uzinduzi wa Hatifungani ya Miundombinu yenye thamani ya Shilingi bilioni 150, iliyopewa jina la "*Samia Infrastructure Bond*". Nawashukuru sana kwa kumwalika Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa mgeni rasmi katika hafla hii. Mheshimiwa Rais aliridhia mwaliko wenu, lakini kutokana na majukumu mengi aliyonayo, amenituma kumwakilisha.

Mhe. Rais anawashukuru sana kwa heshima kubwa mliyompa ya kuwa mgeni rasmi na kutumia jina la lake kuwa sehemu ya historia ya Hatifungani hii, inayoakisi jitihada zake za kuimarisha ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi katika kuharakisha maendeleo. Matumaini yake ni kuwa Hatifungani hii itakuza na kuchochea mwitikio wa wawekezaji, na taasisi nyingine, kutumia chanzo hiki cha fedha katika kutekeleza miradi ya maendeleo yenye gharama kubwa.

**Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki,**

Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya barabara ili kuchochea maendeleo katika sekta mbalimbali, kama tunavyoshuhudia katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Mathalan, mtandao wa barabara za lami nchini umeongezeka kutoka kilomita 13,235.1 mwaka 2020, hadi kufikia kilomita 15,366.36 mwaka 2024. Aidha, bajeti ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imeendelea kuongezeka kutoka Sh. bilioni 414.5 mwaka 2019/20 hadi Sh. bilioni 841.2 mwaka 2024/25. Hata hivyo, mahitaji ya kitaifa ya miundombinu ya barabara vijijini na mijini ni makubwa kwa kuzingatia ukubwa wa nchi yetu, mahitaji ya kukuza uchumi na kuboresha huduma na ongezeko la idadi ya watu. TARURA inakabiliwa na uhitaji wa rasilimali, ikiwa ni pamoja na rasilimali fedha kuweza kuwalipa wakandarasi. Fedha kutoka Serikalini na mapato ya ndani ya TARURA hazitoshelezi.

**Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki,**

Hatifungani inayozinduliwa leo inalenga kuiwezesha TARURA kuongeza mtandao wa barabara za vijijini na mijini kwa kuwashirikisha wawekezaji wa ndani katika ugharamiaji wa miradi ya miundombinu, kukuza ushirikiano na Sekta Binafsi na kuhakikisha ujenzi na ukarabati wa barabara zinazosimamiwa na TARURA, unafanyika kwa wakati ili barabara hizo ziweze kutumika katika kipindi chote cha mwaka. Vilevile, hatifungani hii itasaidia kukabiliana na mahitaji ya dharura ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, unaosababishwa na uharibifu wa mvua kubwa na mafuriko. Taarifa zilizopo zinaonesha kuwa hadi Machi 2024, TARURA ililazimika kutumia takriban Sh. bilioni 50.43 kukabiliana na uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara, ambayo ni zaidi ya mara mbili ya lengo la Sh. bilioni 21.

Vilevile, uwekezaji katika hatifungani hii ni njia mojawapo ya kuiunga mkono Serikali, katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kutokana na ufinyu wa bajeti.

Kwa kutumia fursa hii napenda kuzipongeza kwa dhati taasisi zinazofanya jitihada za kuchochea maendeleo ya Taifa letu kama ambavyo Benki ya CRDB, kwa kushirikiana na OR- TAMISEMI na TARURA walivyobuni Hatifungani hii. Hatifungani hii itawaongezea ukwasi wakandarasi wa ndani wanaotekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara na madaraja, mijini na vijijini.

**Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki**

Katika kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuweka mkazo katika mambo muhimu, yafuatayo:

**Kwanza,** uelewa wa wananchi wetu wengi kuhusu masuala ya fedha na uwekezaji bado ni mdogo. Utafiti uliofanywa na FinScope mwaka 2017 na 2023, unaonesha kuwa watanzania wanaotumia akiba zao kuwekeza katika fursa mbalimbali kama hii ya hatifungani ni 18% tu. Zaidi ya 80% ya Watanzania wanaweka akiba kwa ajili ya dharura na mahitaji muhimu kama elimu, chakula, matibabu na misiba. Hivyo, natoa wito kwa OR-TAMISEMI na CRDB kuhakikisha uzinduzi wa Hatifungani hii unaenda sambamba na utoaji wa elimu kwa umma na kwa lugha rahisi kuhusu masuala ya fedha na uwekezaji katika fursa kama hizi.

**Pili**, hatifugani ya Samia ya Miundombinu ni fursa nzuri ya uwekezaji kwa Watanzania, ambapo moja ya faida zitokanazo na uwekezaji wake ni pamoja na riba ya 12% kwa kila mwaka kwa miaka mitano (5). Pia, riba hii (*coupon*) italipwa kila robo ya mwaka, hivyo kumpatia mwekezaji wa Hatifungani uhakika wa kipato katika kipindi cha kila miezi mitatu. Kiwango cha chini cha uwekezaji kwenye hatifungani hii ni Sh. 500,000 tu, ambacho naamini wananchi wetu wengi wanaweza kumudu. Mathalan, mtu au kikundi kinachoweza kuwekeza Sh. 50,000,000 kitapata kiasi cha Sh. 1,500,000 kila baada ya miezi mitatu, au Sh. 6,000,000 kwa mwaka. Hii ni fursa adhimu ya uwekezaji, hivyo ninahimiza mifuko ya hifadhi za jamii, mifuko ya bima, vyama vya kuweka na kukopa, VICOBA, Makampuni & Taasisi, na mwananchi mmoja mmoja kuchangamkia fursa zinazoambatana na Hatifungani hii.

**Tatu,** wito kwa TARURA ni kubuni na kuongeza matumizi ya teknolojia za kisasa katika ujenzi wa barabara na madaraja ili kupunguza gharama na kuongeza ubora. Aidha, ninawashauri TARURA kutafuta vyanzo vingine vya mapato hususan mikopo ya masharti nafuu ikiwa ni pamoja na ile inayotolewa kupitia dirisha la mabadiliko ya tabianchi na vilevile mchanganyiko wa mikopo na mitaji pamoja na kuingia ubia na sekta binafsi katika kugharamia miradi ya kuendeleza miundombinu vijijini na mijini.

**Nne,** ninawahimiza Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na OR-Mipango na Uwekezaji, pamoja na OR-TAMISEMI, kuweka mfumo wa tahadhari (*early warning system*) utakaowezesha kufuatilia na kubaini mapema vihatarishi vinavyoweza kujitokeza na kuathiri Hatifungani hii ya kimkakati. Vihatarishi hivyo ni pamoja na hali ya ukwasi katika sekta ya benki pamoja na mwenendo wa soko la riba nchini na kimataifa (*interest rate risk*) ambao unaweza kuathiri thamani ya hatifungani ya miundombinu. Aidha,

iwapo miradi ya miundombinu inayogharamiwa kwa utaratibu huu haitatekelezwa kwa wakati, manufaa yanayotarajiwa na wawekezaji yanaweza yasitimie, na hivyo hatifungani hii kupoteza sifa na kuaminika. Hivyo, ninawasisitiza TAMISEMI, TARURA na wakandarasi kuhakikisha ujenzi wa miundombinu imara kwa wakati, na kulingana na thamani ya fedha. Ucheleweshaji, kuongezeka kwa gharama na ubora wa ujenzi pamoja na changamoto za kiufundi na matatizo ya usimamizi ni muhimu yaepukwe kadri inavyowezekana. Vilevile ni vema uwepo mfuko utakaotumika mahsusi kwa ajili ya kulipa riba ya hatifungani na mtaji pale hatifungani itakapoiva.

**Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki,**

Napenda kumalizia kwa kuwapongeza tena OR-TAMISEMI, TARURA, Kamati ya *Samia Infrastructure Bond*, Bodi ya Wakurugenzi na Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB kwa ubunifu na jitihada zenu katika kufanikisha uanzishwaji wa Hatifungani hii. Kadhalika, natoa pongezi za dhati kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Fedha kwa kuhakikisha Hatifungani hii inakidhi vigezo na kuiwezesha kuingia sokoni. Ninawahimiza Mawaziri na Watendaji wengine wa Serikali kuwa wabunifu kwa kuiga mfano mzuri wa Kamati ya *Samia Infrastructure Bond*.

Baada ya kusema haya, ninayo heshima kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, kutamka rasmi kuwa uuzaji wa Hatifungani ya ***Samia Infrastructure Bond*** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara vijijini na mijini, umezinduliwa rasmi.

**Asanteni sana.**